

Maabara ya Taifa ya Kuthibiti Ubora wa Mazao ya Uvuvi

UTANGULIZI


Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imo ndani ya maendeleo ya mifugo na Uvuvi, pia ni mamlaka ya Uthibiti wa ubora wa samaki na mazao yake.

Majukumu yake ni pamoja na kusimamia shughuli zote zinazohusiana na kufuatilia uchakataji wa samaki na mazao yake kwa mujibu wa sheria ya uvuvi, Namba 22 ya 2003 pamoja na kanuni za uvuvi 2009.

Mamlaka hii hutoa huduma za ukaguzi na uchunguzi wa kimaabara ambazo hujumuisha uthibiti, ufuatiliaji wa mazingira pamoja na uhakiki wa samaki na mazao yake ili kukidhi ubora na usalama wa viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

Idara ya maendeleo ya uvuvi kwa sasa inayo maabara moja ijulikanayo kama National Fish Quality Control Laboratory (NFQCL-Nyegezi) yenye sehemu kuu mbili ambazo ni Maabara ya Microbiolojia (Vimelea) na Maabara ya kemikali.

Maabara ya Vimelea imepata ithibati katika aina sita za uchunguzi na maabara ya kemikali, ipo mbioni kutafuta ithibati



MUUNDO WA UONGOZI NA MAJUKUMU YAKE

NFQCL -Nyegezi inaongozwa na afisa mfawidhi wa kanda ya ziwa ambaye husimamia shughuli za utendaji kazi wa maabara wa kila siku Uongozi wa maabara utekeleza kazi na majukumu yake kupitia kamati tatu za uongozi ambazo uendesha vikao vya maamuzi. Kamati hizi ni kamati Kuu ya usimamizi (KKU) kamati ya utendaji wa Maabara (KUM) na kamati ya wataalamu wa maabara ambayo (KWM)

• KKU -Kamati hii hujumuisha mkurugenzi wa maendeleo ya uvuvi Mkurugenzi Msaadizi wa Maendeleo ya Uvuvi, Uthibiti wa viwango na Ubora wa Samaki na Mazao yake na Afisa Mfawidhi wa kanda ya ziwa

- KUM-Kamati hii hujumuisha mkurugenzi msaidizi kwa maendeleo ya uvuvi uthibiti wa viwango na ubora wa samaki na mazao yake na afisa Mfawidhi, Afisa Usimamizi wa Mfumo na Wakuu wa maabara
- KWM- Kamati hii hujumuisha afisa mfawidhi, Afisa Msimamizi wa mfumo, mkuu wa maabara husika, wachunguzi na wachunguzi wasaidizi

DIRA

Kituo cha ubora na mahili katika utoaji wa huduma za upimaji wa vyakula (samaki, mazao ya samaki na mifugo) na vyakula vingine

MALENGO

Kufikia na kuhudumisha hadhi ya ithibati kwa kufata muongozo ISO/IEC 17025, miongozo ya taasisi za uthibitishaji na kutoa huduma zenye kukidhi matakwa ya wateja wetu

MADHUMUNI

- Malengo ya NFQCL -Nyegezi ni haya yafuatayo
- Kuhakikisha huduma za upimaji za maabara zinakua sahihi na majibu yapatikanayo yawe ya kuaminika na kutumainiwa, kutafsiwa, kurudiwa na kulinganishwa.
- Kuanzisha na kudumisha kutambuliwa kitaifa na kitaifa kupitia kufuata vyema matakwa ya muongozo wa ISO/IEC 17025; na taasisi za uthibitishaji.
- Kutimiza mahitaji na kuzidi kiwango cha matarajio ya wateja kwa kutoa majibu sahihi sawia, yakiwa ni maalum na nyeti.
- Kudumisha sifa kwa ubora kwa kuendeleza mchakato wa kuboresha mfumo na kuzuia matatizo.
- Kuendelea kudumisha hali ya ithibati ya NFQCL-Nyegezi




MIPANGO

1) Uchunguzi wa Vimelea

Uchunguzi unaofanywa katika Chakula cha binadamu na mifugo ni Total plate counts, Total coliforms, Enterobacteriaceae, *Staphylococcus aureus*, *Salmonella* spp., *Vibrio cholerae*, *Vibrio parahaemolyticus*, na *Escherichia coli*

Uchunguzi unaofanywa katika kubaini ubora wa maji ni Total plate count at 22 and 37°C, coliform bacteria, *E. coli* and/na *Salmonella* spp.



2) Uchunguzi wa Kemikali

Sehemu hii inayo mitambo yenye kutumia teknolojia ya kisasa na yenye ung'amuzi wa hali ya juu hadi kufikia kipimo cha 10pg/ml au 10pg/kg. Vipimo vya uchunguzi zaidi ya aina 100 vinaweza kufanyika hapa kutoka katika sampuli za vyakula vya mifugo, madini na ufuatiliaji wa kimazingira

Chunguzi hizi zinaganywa katika makundi haya yafuatayo; Uchunguzi ya mabaki ya viuatilifu, Uchunguzi wa Madini tembo, Uchunguzi wa sumu katika vyakula na Uchunguzi wa viwango na aina za virutubisho katika chakula



3) Huduma ya ukaguzi na uhakiki kwenye viwanda vya vyakula na maabara.

4) Kuratibu na kuendesha mafunzo ya ISO 17025, ISO 9001 series, ISO 22000, HACCP n.k.

5) Huduma ya utafiti na ushauri NFQCL-Nyegezi inashirikiana na Vyu vikuu, vyuo vya mafunzo na taasisi za utafiti pamoja na mashirika binafsi (NGOs) kufanya utafiti na ushauri mabalimbali katika sekta ya chakula cha binadamu na mifugo.



6) Miradi wa TASP II

Miradi huu unalenga kupunguza umasikini wa wavuvi na wafanyabiashara wa samaki kwa kukuza na kuongeza kipato chao, kuhakikisha upatikanaji endelevu wa samaki, kuongeza ubora na thamani ya mazao ya uvuvi hususani mazao ya dagaa kutokana na kuboresha njia za usindikaji, pia kuhakikisha usalama kwa mlaji wa mazao ya dagaa.

Kutokana na kuboresha mazao ya dagaa itatoa nafasi kwa uhindani wa kibiashara katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Miradi wa TASP II unatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo: Kuimarisha weledi wa wafanyakazi pamoja na vifaa na mashine za uchunguzi.

Kuimarisha uelewa wa wavuvi na wafanyabiashara ya dagaa katika ubora na usalama wa mazao ya dagaa ili kulinda afya ya mlaji pamoja na kudumisha soko la dagaa ndani na nje ya nchi. Pia na kuboresha usafi, ubora, uhudumiaji, uchakataji na ufungashaji wa zao la dagaa kwa ajili ya kudumisha soko la ndani na nje ya nchi.

WADAU

NFQCL -Nyegezi inawakaribisha na inatoa huduma kwa wateja wa ndani na nje ya nchi.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
Mkurugenzi wa Uvuvi
S.L.P 2462

DAR ES SALAAM
Afisa Mfawidhi wa Kanda ya Ziwa
S.L.P 1213
MWANZA

Simu: +255 28 2550864
Nukushi: +255 28 2550025

Simu: +255 754/784 437234
Barua Pepe: nfqcl_mz@yahoo.co.uk

Tovuti: www.nfqcl.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI



MAABARA YA TAIFA YA UTHIBITI WA MAZAO YA UVUVI NFQCL-NYEGEZI

Mpango Mkakati wa Kuimarisha na Kukidhi
Ubora na Viwango vya Samaki na Mazao yake



TRADE AND AGRICULTURE
SUPPORT PROGRAMME II
(TASP II)